**OFISI YA RAIS TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MJI KONDOA**
**JARIDA LA HALMASHAURI**

Toleo Na. 2

Julai 2018— Machi 2019

# Mapato ya Hospitali Ya Kondoa Mji Yaboresha Huduma Za Maabara




## SERA YA UHARIRI

Madhumini ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

**Bodi ya Uhariri**

Msoleni Dakawa

Sekela Mwasubila

Godhard Hunja

Abdul Omary

**Mawasiliano**

S.L.P 711 Kondoa

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

**Mitandao ya Kijamii**

www: kondoatc.go.tz

Kondoa TC

kondoatc2015

KondoaTC

@KondoaTC

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz

# NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



Msoleni Dakawa
Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa

Natoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniteua kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa tarehe 13.08.2018.

Pia natoa shukrani kwa Waziri wa TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Mahenge kwa uongozi mzuri na uwajibikaji pamoja na shukrani hizo pia namshukuru Mhe. Sezaria Makota Mkuu wa Wilaya ya Kondoa , Mhe. Hamza Mafita Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Mhe. Edwin Sannda Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini.

Halmashauri ya Mji Kondoa imejipanga kutoa huduma bora kwa watumishi na wananchi kwa ujumla kwa kuzingatia Misingi ya Utawala Bora na uwajibikaji .

Hata hivyo Halmashauri imeweza kutatua kero nyingi za wananchi ambazo awali walikuwa wanazipeleka mkoani Dodoma na OR– TAMISEMI kwasasa kero zote zinatatuliwa katika ngazi ya Mji, Kata na Mitaa.

Hata hivyo Halmashauri ya Mji wa Kondoa imeweza kufikia asilimia 97.3 ya makusanyo ya mapato ya ndani hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi 2019, hii ni kutokana na ushirikiano wa timu ya Wakuu wa Idara na Watumishi wengine kwa kufanya operesheni ya mapato kila Jumatano na Ijumaa ya kila wiki.

Pia kwa kipindi cha miezi tisa Julai hadi Machi Halmashauri imenunua mashine 10 za kukusanyia mapato POS(Point Of Sale) ambapo mpaka sasa Halmashauri ina mashine 45, kati ya hizo 20 tumepewa na shirika la LIC (Local Investment Climate).

Mwisho, mpango uliopo ni kuzidi kuongeza mapato ya ndani kwa kubuni vyanzo vipya vya ili kuendelea kuboresha na kutoa huduma kwa wananchi, lengo likiwa ni kuipandisha hadhi Halmashauri ya Mji na kuwa Halmashauri ya Manispaa siku za usoni.

**ASANTENI SANA**

JIPATIE NAKALA YA GAZETI HILI KWA KUPAKUA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI YA MJI KONDOA

www.kondoatc.go.tz

# BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI



Mhe. Hamza Mafita
Mwenyekiti wa Halmashauri



Mhe. Edwin Sannda
**Mbunge Kondoa Mjini**



Mhe. Zainabu Haroub
**M/Mwenyekiti wa Halmashauri**



Mhe. Kipaya Mdachi
**Diwani kata ya Chemchem**



Mhe. Abushehe Mbuva
**Diwani Kata ya Kingale**




Mhe. Ally Modu
**Diwani Kata ya Suruke**



Mhe. Besela Maunga
**Diwani V/M Kondoa Mjini**



Mhe. Abeid Boki
**Diwani Kata ya Bolisa**




Mhe. Ramla Abeid
**Diwani V/M Bolisa**



Mhe.  Issa Kambi
**Diwani Kata ya Kilimani**



Mhe. Ezekiel Afande
**Diwani Kata ya Serya**



Mhe. Salimu Maguo
**Diwani Kata ya Kolo**

# MAPATO YA HOSPITALI YABORESHA HUDUMA ZA MAABARA

Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kondoa imekarabati jengo la maabara hali iliyopelekea kuboreshwa kwa huduma za vipimo katika hospitali hiyo.

Hayo yamebainishwa na Mganga Mkuu wa Halmashauri Dkt. Eusebi Kessy alipokuwa akiongelea ukarabati wa maabara hiyo ofisini kwake hivi karibuni.

Alisema kuwa ukarabati huo umefanyika kwa kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya hospitali yatokanayo na uchangiaji wakati wa kutoa huduma mbalimbali hospitalini hapo.

"Ukarabati huu umefanyika katika maeneo matano ikiwemo kubadilisha muundo wa jengo kutoka wodi hadi muundo wa maabara, kujenga eneo la wagonjwa kusubiria majibu, kusogeza huduma ya vyoo katika jengo hilo kwa ajili ya wagonjwa,kujenga mfumo wa maji safi na maji taka na kubadilisha mfumo wa umeme."Alisema Dkt.Kessy

Aidha aliongeza kuwa ukarabati huo umepelekea kuongezeka kwa baadhi ya vipimo ambavyo hapo awali havikuwepo ikiwa ni pamoja na kupima kifua kikuu kwa vina saba ambapo mashine ilikuwepo na ilikuwa haitumiki ikiwa ni sambamba na kuanzisha kipimo cha uoteshaji wa vijidudu ambavyo vitapelekea kupatikana kwa majibu sahihi na kwa wakati sahihi na kuongeza mapato ya hospitali.

Kwa upande wake msimamizi wa maabara hiyo Daud Maswaga alisema kuwa wagonjwa wamefurahia maboresho yaliyofanyika kwani awali walikuwa wakipata shida kukaa kwenye jua na kunyeshewa na mvua msimu wa mvua.

"Lakini pia kwa upande wa vipimo tumeboresha tumeongeza vifaa vya kupimia ambavyo vilikuwa vikihitaji sehemu salama lakini pia uboreshaji huu umeongeza usalama kwa wataalam wa maabara na kupunguza hatari ya kupata maambukizi". Alisema Maswaga

Mmoja wa wagonjwa aliyekuwa akisubiria huduma katika maabara Bi. Fransisca Haule alisema kuwa wanafurahia maboresho yaliyofanyika na kuomba uongozi kuboresha na maeneo mengine ili wananchi wapate huduma bora.




Wataalam wa maabara katika hospitali ya mji Kondoa wakiendelea na kazi katika maabara iliyoboreshwa.

SERIKALI YA AWAMU YA TANO IMEJIPANGA

KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA KATIKA

NYANJA ZOTE SABABU MTU NI AFYA.



Wagonjwa wakisubiri kupata huduma nje ya jengo la maabara kabla ya kufanyiwa ukarabati

# WIZARA YA AFYA YAWAPONGEZA HEAD INC



Mkuu wa wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota (wa nne kutoka kushoto) akiwa katika picha ya

Wizara ya Afya imelipongeza Shirika la Head Inc lenye Diaspora wa Kondoa kutoka nchini Marekani kwa kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano katika masuala ya afya.

Pongezi hizo zimetolewa na Dkt. Dorothy Gwajima kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya wakati wa ufunguzi wa zoezi la kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Kondoa zitakazotolewa na madaktari bingwa kutoka shirika hilo.

"Serikali ya awamu ya tano imeendelea kuboresha huduma za afya kila siku na wenzetu hawa Diaspora wameliona hilo na wakaona ni vema kuunga mkono jitihada hizo kwa kuja kutoa huduma hii nyumbani tunawashukuru sana na naamini mnaweza kusaidia katika maeneo mengine kwa kutoa elimu kwa wataalam wetu wa afya."Alisema Dkt. Gwajima

Aliongeza kuwa kuna michakato mingi hadi walipofika Kondoa hasa maeneo ya bandarini na katika Taasis zingine za serikali ili kuingiza vifaa vyenu lakini hilo linafanyika katika kuhakikisha kuwa dawa na vitu vingine vinakuwa katika ubora na viwango vinavyotakiwa nchini na kuahidi kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuanzisha dawati litakalokuwa

linashughulikia masuala ya Diaspora na kupunguza michakato hiyo.

"Nashauri uongozi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji kutengeneza Mpango Mkakati wa kuboresha huduma za Afya na kuwapatia wenzetu hawa ili wakifika huko Marekani wanaweza kuona jinsi ya kutusaidia ikiwemo kuboresha huduma za wagonjwa mahututi."Alishauri Dkt. Gwajima

Akiongea katika ufunguzi huo Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota aliwashukuru wadau hao kwa msaada walioutoa na kuwasihi wananchi kutumia fursa hiyo kwa kuwataarifu wengine na kujitokeza kwa wingi kwani zoezi hilo ni kama lililofanyika mwaka jana na litawasaidia wananchi kuondokana na maradhi.

Hata hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa akitoa salamu za shukrani alisema kuwa ujio wa Diaspora hao umetokana na kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. John Magufuli katika upande wa Afya ambapo pia ametoa kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Kingale.

Ujio wa Diaspora katika Halmashauri ya Mji Kondoa umewezeshwa na shirika la Head Inc kutoka nchini Marekani ambapo watatoa huduma ya afya katika Hospitali ya Mji Kondoa kwa muda wa siku nne kwa magonjwa ya kinywa na meno,magonjwa ya kinamama,magonjwa ya watoto na magonjwa ya macho.



# "KINGALE SHIRIKIANENI" – DKT MAHENGE



Mbunge wa Kondoa Mjini Mhe. Edwin Sannda akisisitiza jambo mbele ya mkutano wa Mkuu wa Mkoa Dkt. Binilith Mahenge na wananchi wa Kata ya Kingale alipotembelea katika eneo litakapojengwa kituo cha Afya

Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Dkt. Binilith Mahenge amewataka wananchi wa Kata ya Kingale kushirikiana pamoja katika ujenzi wa Kituo cha Afya Kingale kwani huduma zitakazotolewa zitawanufaisha wote.

Aliyasema hayo wakati wa ziara yake katika Kata ya Kingale eneo linalojengwa kituo cha Afya na kufanya mkutano wa hadhara hivi karibuni.

"Fedha zimetolewa Na Rais Dkt John Magufuli kwa ajili ya kuboresha huduma za Afya jambo ambalo litawapunguzia umbali wa kufuata huduma mjini kwa kumuunga mkono Rais shirikianeni kukamilisha kituo hiki."Alisema Dkt. Mahenge

Aliongeza kwa kuwataka viongozi wa Mitaa ambayo haijachangia kwenda kuitisha mikutano na kuwahamasisha wananchi kuchangia ujenzi kama Mitaa mingine kwani ugonjwa ukija hauangalii chama, urefu wala kabila la mtu.



Wananchi wa Kata ya Kingale wakijitolea nguvu kati katika ujenzi wa Kituo cha Afya Kingale

Awali akiongea katika mkutano huo Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe.Sezaria Makota alisema kuwa wananchi wa Kingale ni wapenda maendeleo pia ni moja ya Kata zinazoongoza katika Elimu na uchangiaji wa CHF na juhudi zao zimeonekana katika ujenzi wa Kituo cha Afya ambapo wameshachangia tofali, mchanga na mawe ambavyo vipo eneo la ujenzi tayari.

## UMOJA NI NGUVU

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi Issa Ramadhan alisema kuwa mradi huo uliibuliwa na wananchi na jumla ya majengo matano yatajengwa ikiwemo nyumba ya mganga ambapo Serikali imetoa jumla ya Shilingi Milioni 400 na wananchi wanatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 15 na hadi sasa wamechangia shilingi milioni 11.

# KONDOA MJI YAPONGEZWA KUZINDUA BARAZA LA WAFANYAKAZI

Halmashauri ya Mji wa Kondoa imepongezwa kwa kufanya uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi ikiwa ni Halmashauri ya pili katika Mkoa wa Dodoma kufanya hivyo.

Pongezi hizo zilitolewa na Katibu Tawala wa Wilaya Andrea Ng'wani wakati akizindua Baraza hilo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya uzinduzi uliofanyika katika ukumbi wa Kondoa Irangi Kondoa Mjini.

Alisema kuwa Baraza hilo likawe chombo cha kusema katika kufikisha matakwa ya watumishi na kuimarisha ushirikiano na mwajiri na kuwa ana uhakika katika Baraza hilo wajumbe watawasilisha wanayoona yatafaa katika kushirikiana na mwajiri kutatua changamoto za kazini.

"Mnaweza mkaona katika uongozi huu wa awamu ya tano jinsi Mheshimiwa Rais anavyofanya mabadiliko ya kuiendeleza nchi na wakuyafanya haya ni sisi wafanyakazi hivyo kila mmoja awajibike katika eneo lake na kujitathmini ili tuendane na upepo uliopo."Alisema Ng'wani

Aidha alisisitiza wafanyakazi kufanya kazi na kutimiza majukumu yao walioajirwa nayo kwa asilimia zote pamoja na melekezo wanayopewa kwani kwa kufanya hivyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais, Mkuu wa Wilaya, Halmashauri na wananchi wanaowahudumia.

Aidha kwa upande wake Mkurugenzi wa Mji Kondoa Msoleni Dakawa alisema kuwa Baraza limeanzishwa baada ya kuona umuhimu wa wafanyakazi kwa kuwa katika Serikali mfanyakazi ndio mzalishaji na mtekelezaji wa maagizo na ahadi zinazotolewa na Serikali.

"Niombe kwa wakati mwingine kwa umoja huu tuliouonesha na vyama vya wafanyakazi tuendelee nao iwe wakati wa shida na raha kwani lengo ni kuhakikisha mambo yanaenda na tuna wajibu wa kupambana kama anavyofanya Mheshimiwa Rais lengo likiwa kuwahudumia wananchi na kuwapatia haki zao watumishi." Alisisitiza Dakawa

Naye mwakilishi wa vyama vya wafanyakazi ambaye ni Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma Bwana Mchenya John alisema kuwa Baraza la Wafanyakazi ni chombo muhimu cha maamuzi kwa Halmashauri na kuwataka wajumbe wa Baraza kuacha uoga na kujadili mambo yatakayowasaidia kuendesha Halmashauri na maslahi ya watumishi.

"Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulitolea maamuzi suala la kikokotoo kwani liliwakatisha tamaa sana wafanyakazi."Alimaliza Bwana Mchenya.



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Halmashauri ya Mji Kondoa wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa vyama vya wafanyakazi kutoka mkoa wa Dodoma na Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa.

# "Endelezeni Rekodi ya Ufaulu" - Mhe. Sannda



Mkuu wa Shule ya Sekondari Gubali Yusuph Kijuu kushoto akisoma taarifa ya shule mbele ya Mhe. Edwin Sannda Mbunge wa Kondoa Mjini

Wanafunzi wa kidato cha pili na nne Shule ya Sekondari Gubali wamehimizwa kuendelea kusoma kwa bidii, maarifa na kuongeza juhudi ili kuendeleza rekodi yao ya ufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Hayo yalisemwa na Mbunge wa Kondoa Mjini Mhe. Edwin Sannda alipokuwa akizindua kambi ya kitaaluma kwa wanafunzi wa kidato cha pili na cha nne katika shule ya Sekondari Gubali alipofanya ziara shuleni hapo hivi karibuni.

"Wanafunzi nataka msome kwa bidii sana na kikubwa ni kuwa na nidhamu ili baadae mje kuwa Madaktari, Marubani, waalimu na Wahandisi mkatujengea majengo yetu na kuwa na maisha mazuri." Alisema Sannda

Aliendelea kwa kuwaahidi kuendeleza utaratibu wa ofisi yake ya kuwasomesha wanafunzi watakaofaulu kwa daraja la kwanza mtihani wa kidato cha nne kwa kuwalipia ada na matumizi kwa kidato cha tano na sita.

Aliendelea kufafanua kuwa lengo kuu la kuwasomesha wanafunzi hao ni kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano ambapo elimu hutolewa bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne hivyo kuwapunguzia mzigo wazazi kwa kulipa ada ya kidato cha tano na sita ofisi yake inatekeleza hilo kwa watakaopata daraja la kwanza na mwisho akienda chuo atapatiwa mkopo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa Mhe. Hamza Mafita aliwapongeza wanafunzi hao kwa rekodi nzuri ya ufaulu na kusema kuwa Halmashauri itaendelea kuwaboreshea mazingira ya kujifunza na kujifunzia.

# WATENDAJI WATAKIWA KUFANYIA KAZI MAAGIZO WANAYOPEWA



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Msoleni Dakawa (aliyesimama) akisisitiza jambo wakati wa kikao kazi kati ya watendaji wa Kata na Mitaa (hawapo pichani) pamoja na Wakuu wa wa Idara. Wa kwanza kutoka kushoto Bwana Dickson Mwangwegho Mkaguzi wa Ndani, Bi. Kaunga Amani Afisa Mipango na Bi. Lucy Timba Afisa Utumishi

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa Msoleni Dakawa amewataka watendaji wa kata na mitaa kuyafanyia kazi maagizo yanayotolewa kutoka Halmashauri kwani wananchi wana imani nao katika kuwaletea maendeleo.

Aliyasema hayo wakati akifungua kikao kazi kati ya watendaji hao na wakuu wa Idara kilichofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Uwekezaji Kondoa Mjini.

Alisema kuwa watendaji hao ndio wasimamizi na Wakurugenzi katika maeneo yao ya kazi hivyo wanapaswa kuwajibika ili kuhakikisha kata na mitaa yao inakuwa na maendeleo na huduma za msingi zinapatikana.

“Mkifanya vibaya nyie Halmashauri yote itaonekana imefanya vibaya sababu tunafanya kazi kama timu ila nasikitika watumishi ngazi ya wilaya wanafanya sana kazi lakini ikifika kwenu hamfanyi kazi na kutimiza majukumu yenu mjitathmini.”Alisema Dakawa

Aidha aliongeza kwa kuwataka kusimamia miradi ya maendeleo na ukusanyaji wa mapato na kuwachukulia hatua wale wote ambao miradi itatekelezwa chini ya kiwango na wao kutochukua hatua zozote kwa kisingizio cha kutokushirikishwa kwani miradi yote ipo chini yao.

“Pia kuna watendaji hapa nimepata habari ni wababe kwa wenyeviti wao wa mitaa hadi wanaogopwa hii haipendezi mkafanye kazi kwa kushirikiana lengo liwe moja tu kuwaletea maendeleo wananchi.” Alisisitiza Dakawa

Kwa upande wake Afisa Sheria wa Halmashauri Wakili Edward Mhina aliwataka watendaji kuepuka tabia ya kuingia mikataba na watu mbalimbali bila kushirikisha ofisi ya Mkurugenzi kwani mikataba yote ambayo haijapitiwa na Mwanasheria ni batili.

“Nawakumbusha watendaji ambao walipewa mashine za kukusanyia mapato na hawakupeleka fedha benki kufanya hivyo ndani ya wiki moja hadi jumatano ijayo wote wapeleke fedha benki ambao hawatapeleka tutawafikisha mahakamani.”Alisema Mhina

Akiongea kwa niaba ya watendaji Mtendaji wa Kata ya Kingale Samson Mtui aliushukuru uongozi wa Halmashauri kwa kikao kazi hicho kwakuwa kimewakumbusha majukumu yao ambayo mengi walikuwa wakiyafanya .

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa Mhe. Hussen Mwinyi akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa wilaya ya Kondoa alipotembelea Wilayani humo.



Moja kati ya matanki 5 ya maji yaliyowekewa miundombinu ya usambazi wa maji Kondoa Mjini katika baada ya kupata fedha



Bweni la Shule ya Wasichana Kondoa likiwa katika mwonekano mpya baada ya kuewa fedha na serikali katika mpango wa ukarabati wa shule kongwe nchini.



Mwonekano wa baadhi ya majengo ya Kituo cha Afya Kingale kinachoendelea kukamilishwa baada ya Serikali ya awamu ya tano kutoa shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa



Mafundi wanaojenga jengo la Halmashauri ya Mji Kondoa wakiendele na ujenzi wa jengo kabla ya kuanza ujenzi wa kuta hizo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa (wa tano kutoka kushoto)akiwa na viongozi wa Chama Cha Maafisa Mawasiliano Tanzania (TAGCO) walipotembelea ofisini kwake.

# TANGAZO LA UUZWAJI WA VIWANJA KATIKA MAENEO YA UBEMBENI NA KICHANGANI—HALMASHAURI YA MJI KONDOA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA HALMASHAURI INAUZA VIWANJA KATIKA MTAA WA UBEMBENI NA KICHANGANI. FOMU ZA MAOMBI ZINAPATIKANA KATIKA JENGO LA KITUO CHA BIASHARA LILILOPO KARIBU NA BENKI YA CRDB KWA BEI YA TSHS. 20,000/= AMBAYO HAITARUDISHWA.

VIWANJA VINAVYOUZWA NI VYA MAKAZI NYENYE UJAZO WA JUU (HIGH DENSITY), KATI (MEDIUM DENSITY) NA CHINI (LOW DENSITY) NA VIWANJA VINGINEVYO VYA MATUMIZI MBALIMBALI YA HUDUMA ZA KIJAMII.

## BEI YA KIWANJA KWA MITA MOJA YA MRABA

| \NA | MATUMIZI | BEI YA KIWANJA KWA MITA MOJA YA MRABA (TSHS/1METER SQUARE) |
|---|---|---|
| 1 | Makazi Pekee ( Residential) | 2,500/= |
| 2 | Makazi na biashara (Commercial Residential) | 3000/= |
| 3 | Biashara pekee (Commercial) | 4000/= |
| 4 | Makazi ya pamoja (Housing Estate) | 6000/= |
| 5 | Hoteli (Hotel Site) | 10,000/= |
| | | |

MUDA WA KULIPIA KIWANJA NI MIEZI SITA AMBAPO NDANI YA MWEZI BAADA YA MTEJA KUPEWA KIWANJA ANATAKIWA KULIPA NUSU YA GHARAMA YA KIWANJA HICHO NA KABLA YA KUISHA MIEZI SITA ANATAKIWA KUWA AMEMALIZA DENI LOTE NA ATAKAYESHINDWA KUMALIZA KIWANJA ATAPEWA MTU MWINGINE NA YEYE ATAKATWA ASILIMIA 20 YA FEDHA ALIYOTOA .

**WOTE MNAKARIBISHWA**

LIMETOLEWA NA

MSOLENI DAKAWA

**MKURUGENZI KONDOA MJI**